JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA

## TAARIFA KWA WAOMBAJI WALIOSHINDWA KUTUMA MAOMBI YA UDAHILI WA SHAHADA YA KWANZA KWA MWAKA WA MASOMO 2026/2027

Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) imepokea maombi kutoka kwa baadhi ya waombaji wa udahili, hususan wenye sifa za Stashahada ambao kutokana na kuchelewa kupata Namba za Utambuzi wa Tuzo (AVN), walishindwa kutuma maombi ya udahili wa Shahada ya Kwanza katika Awamu ya Kwanza na ya Pili.

Tume inapenda kuwataarifu waombaji wote kuwa imeweka utararibu maalumu utakaowapa fursa ya kutuma maombi ya udahili. Utaratibu huo, pamoja na muda wa kutuma maombi, utatangazwa tarehe 6 Oktoba 2026 wakati wa kutangazwa kwa majina ya waombaji waliodahiliwa katika Awamu ya Pili.

Hivyo, Tume inawasihi waombaji wote ambao kwa sababu mbalimbali, hawakuweza kutuma maombi ya udahili katika Awamu ya Kwanza na ya Pili, kufanya maandalizi muhimu mapema. Maandalizi hayo yanajumuisha kuhakikisha kuwa waombaji wenye sifa za Stashahada wanakuwa na AVN ili waweze kutumia ipasavyo fursa hiyo itakapotangazwa.

Tume inawashauri waombaji wa udahili na wadau wengine kuendelea kufuatilia taarifa rasmi zinazotolewa kupitia tovuti na njia rasmi za mawasiliano za TCU.

Imetolewa na:

**Prof. Charles D. Kihampa**

**KATIBU MTENDAJI**

24/9/2026